*Msururu wa mwongozo wa mazoez za CTA, Nambari 13*

# Jinsi ya kufuga nyuki na kuchakata asali



CTA

# Jinsi ya kufuga nyuki na kuchakata asali

Asaf Ayatuhaire, kutoka wilaya ya Bushenyi, Kusini-magharibi mwa Uganda, ana zaidi ya mizinga 100 ya aina mbali mbali. Huzalisha asali yapata kilo 2000 kila mwaka, na kupata zaidi ya dola 2,200 za marekani kwa mwaka. Hivi majuzi aliisajili kampuni yake kwa jina West Honeys Uganda.



*Asali iliyorinwa muda mfupi uliopita*

Lakini miaka kumi iliyopita, Asaf alikuwa na mizinga mitatu tu ya kienyeji na alipata kilo sita tu za asali kwa mwaka. Baadae, alihudhuria warsha ya kitaifa ya kufunza wakufunzi iliyoandaliwa na kudhaminiwa na idara ya entomolojia ya wizara ya kilimo nchini humo. Baada ya kukamilisha mafunzo yake, alijihusisha na kuwafunza wafugaji wa nyuki katika eneo lake. Asaf pia aliweza kukutana na kushirikiana na mashirika yasiyo ya serikali, mashirika ya kimataifa na kitaifa vya kutoa ufadhili kama vile USAID, FAO na Kikundi cha wakulima wilayani. Vikundi hivyo vilimsaidia kupanua bustani yake ya nyuki na kupata mizinga ya kisasa.





Leo, kwa sababu ya ufugaji nyuki, Asaf ana nyumba ya kisasa, analipa karo ya wanawe katika shule za sekondari na elimu ya juu na pia anaweza pia kujiwekea akiba.



### Kwa nini ufuge nyuki?

- Nyuki huchavusha mimea ya mazao mashambani na hivyo basi kuboresha mavuno.
- Soko kubwa la asali linapatikana mitaani, kitaifa na kimataifa.
- Maji maji yanayokusanywa kutoka kwenye mimea na nyuki kufunika ndani ya mizinga, hutibu maradhi aina mbali mbali.
- Chavu iliyokusanywa kwenye mimea na nyuki kulisha watoto wao wachanga, inatumika katika sekta ya utengenezaji manukato, ni kiungo cha kuongeza ladha katika chakula na pia dawa.
- Maji maji kama kamasi yaliyotengenezwa na nyuki wachanga kutoka tezi na kumlisha malkia kumfanya awe na nguvu yana manufaa kama dawa.

- Nta hutumiwa katika vipodozi, mishumaa na rangi za viatu.
- Uanzishaji wa kufuga nyuki unahitaji nafasi ndogo na gharama yake ni ndogo.
- Karibu asili mia 80 ya asali ina sukari ambayo huchukuliwa na mwili kwa haraka hivyo basi kuifanya bora kwa watoto, wagonjwa na wale wanaofanya kazi nzito (kazi za sulubu).

## Uchaguzi wa mzinga unaofaa

| Aina ya mzinga | Manufaa | Ubaya |
| --- | --- | --- |
| Mzinga wa kiasili ulioshonwa<br> | Ni wa bei nafuu na rahisi kujenga<br>Inatengenezwa kutoka kwenye vitu vinavyopatikana kwenye maeneo yetu tunamoishi<br>Maji maji ya nyuki huwa mengi zaidi kuliko aina zingine za mizinga. | Nyuki hawawezi kukaguliwa<br>Ni vigumu kuzuia nyuki wengi kutangama na kuuzunguka mzinga huo ama kubadilisha malkia<br>Ubora hauwezi ukadhibitiwa vilivyo kwa sababu masega ya nyuki yaliyo na mabuu hayawezi kutenganishwa na ile yenye asali<br>Mavuno ya asali yako chini (kati ya kilo sita na kumi kila mwaka)<br>Mzinga hudumu hadi miaka miwili tu |

| Aina ya mzinga | Manufaa | Ubaya |
|---|---|---|
| Mzinga wa *top bar*  | Unaweza kutengenezwa kwa kutumia vifaa vipatikanavyo kwa urahisi na pia ni vya bei nafuu<br>Ni rahisi kukagua nyuki na kudhibiti nyuki wengi wanaotangamana<br>Ubora wa asali unaweza kuchunguzwa<br>Hutoa kilo 20 hadi 40 kwa mwaka<br>Hudumu hadi miaka 10<br>Waweza pata nta zaidi kwa sababu sega hukatwa kwa lazima kutoka kwenye kuta za ndani za mzinga asali inaporinwa | Ni ya bei ya juu kuliko mzinga wa kienyeji<br>Ni vigumu kwa mkulima mdogo kupata kiasi wastani kinachostahili ili kupata faida (kama mizinga 10 hivi)<br>Maadui na wadudu wengine wanaweza kufikia mizinga kwa sababu inaning'inia karibu na ardhi |
| Mzinga wa *Langstroth*  | Sega zenye nta zaweza kutengwa na zile zenye asali<br>Uzalishaji ni kati ya kilo 50 na 60 kwa mwaka<br>Ubora wa asali unaweza kuchunguzwa | Ni bei ghali kutengeneza ama kununua<br>Unahitaji mtu mwenye ujuzi mwingi kurina asali hiyo kutoka kwenye masega<br>Yahitaji ujuzi zaidi wa kufuga nyuki |

### Uchaguzi wa sehemu ya kufuga nyuki

Mizinga ya nyuki inafaa kuwekwa karibu na maji (mito, vijito, madimbwi, ziwa, mabwawa na kadhalika) katika sehemu iliyo na uoto wa kutosha kama kahawa, alizeti, mninga, miembe, michungwa, migomba na mimea mingine inayotoa maua.

Sehemu hii inapaswa kuzungukwa na ua ili kuwalinda nyuki kutokushambulia watu na wanyama wengine (na watu na wanyama kutokana na mashambulizi ya nyuki).

Mizinga inafaa kuwekwa umbali wa mita 30 au zaidi hivi kutoka barabarani, sehemu za umma au zenye kelele nyingi kama soko na shule.

### Kuongeza idadi ya nyuki katika mizinga

Kuna njia mbili za kuongeza idadi ya nyuki.

#### 1. Kuvutia nyuki

- Tumia mzinga mdogo ulitumika na nyuki hapo awali uijaze na fremu ama sehemu za juu; fremu mbili zapaswa kuwa na masega na zingine zapaswa kuwa na shiti za nguzo ama michirizi ya masega yaliyotumika.
- Weka mzinga huo kwenye mti ama juu ya paa kuizuia dhidi ya upepo.
- Weka mzinga mahali panapofaa siku ile nyuki wahamiapo kwenye mzinga huo.
- Kuvutia nyuki ni muhimu wakati wa msimu wa kuhamia, kwa kawaida ni mwanzoni mwa msimu wa kiangazi ama mwisho mwa msimu wa baridi.

#### 2. Kuwateka nyuki

- Waweza kuwateka nyuki waliohamia kwenye tawi la mti, lakini hakikisha umevaa nguo zifaazo ili kujikinga.
- Nyunyizia maji baridi kwanza juu ya nyuki kwa kutumia brashi ama chupa ya kunyunyizia ili kuwazuia kuhama.
- Shika mzinga mdogo usiokuwa na fremu, kikapu ama sanduku chini yao.
- Wahamishe nyuki katika mzinga kwa kutumia brashi au moshi.

**Urinaji/Uvunaji wa asali**

Kwa mizinga ya kienyeji ama aina ya top bar, rina/vuna asali mara mbili kwa mwaka. Kwa mzinga wa *Langstroth*, rina/vuna mara tatu ama nne kwa mwaka.

**Njia ya kuirina asali:**

- Vaa nguo za kujikinga kama ovaroli, utaji, glavu, buti.
- Kipuliza moshi.
- Fungua mzinga taratibu.
- Chagua sega zilizofunikwa na asali theluthi mbili.
- Epuka sega zilizo na mabuu.
- Inua sega, puliza moshi pande zote mbili kisha waondoe nyuki taratibu ukiwarudisha mzingani kwa kutumia manyoya.
- Kata masega yote ukibakisha sentimita moja kwenye mbao.
- Tia asali iliyorinwa mahali safi, pakavu kwenye konteina kisha utie kifuniko.
- Acha sega zisizopungua nane kwa nyuki.
- Kabla ya kufunga mzinga, sukuma sega zisizokomaa karibu na ile sega iliyo na mabuu kisha utie mbao nyuma yao.



1 *Kujitayaraisha*



2 *Hatua za kurina asali*


**Kuchakata asali**

- Tumia chuma au kisu moto kuifungua sega (kwa kuipitisha juu ya sega).
- Tia sega iliyofunguliwa juu ya kitambaa cheupe kisafi. Upande uliowazi unapaswa kuangalia chini.
- Acha asali itiririke kutoka kwenye seli hadi iishe.

- Geuza sega kisha urudie mpangilio huo.
- Tia asali katika chupa na ufunike vizuri. Weka tarehe kisha uhifadhi mahali pakavu na pasipo na joto.

### Kuweka kumbu kumbu

Ni muhimu kuweka kumbu kumbu kila unapokagua ili kuchunguza jinsi koloni ilivyo na kufuatilia hali zao. Mizinga inafaa kukaguliwa mara mbili au tatu kwa mwezi. Waweza kutumia mada zifuatazo unapokagua: namba ya mzinga, tarehe ya nyuki kuhamia, tarehe ya ukaguzi, uchunguzi, uzalishaji kwa mwezi katika kilo.



❸ *Asali ilirinwa kwenye sega*



❹ *Kupakia asali kwa mauzo*

| **Nini chaweza kwenda mrama?** | **Sababu/Chanzo** | **Suluhisho** |
|---|---|---|
| Nyuki kuhama | Ukosefu wa maji na chakula<br>Usumbufu wa mizinga k.m. kwa moto, maji ama wanyama<br>Uvamizi wa mara kwa mara na wadudu ama vimelea. | Hakikisha kuna chakula cha kutosha: panda maua karibu na mizinga<br>Hakikisha masega siyo makubwa sana kwa kuvuna mara kwa mara yanapokuwa yamejaa<br>Weka maji karibu wakati wa ukame<br>Punguza ukubwa wa koloni<br>Weka mzinga umbali usiopungua mita 30 kutoka kwenye barabara na sehemu za umma na mahala na uweke ua<br>Uwatunze kwa utulivu unapowakagua<br>Hakikisha usafi katika sehemu uliyoweka mizinga |
| Nyuki kukuuma | Kusumbuliwa kwa mzinga | Kuwa mtulivu, ondoa usena/ mshale kisha puliza moshi kwenye sehemu hiyo<br>Ukizidiwa nenda katika kliniki ama hospitali iliyo karibu nawe |
| Wadudu waharibifu (siafu, mchwa, mhilu) | Utunzaji mbaya wa mizinga | Weka mizinga katikati ya miti<br>Fito zikitumika, zipake kwanza mafuta ya mashine yaliyotumika au grisi ili kuzuia mchwa na siafu |
| Kutumia dawa zinazowaua nyuki za kunyunyiza | Kunyunyizia dawa ya kemikali karibu na mizinga | Wasiliana na wakulima wengine ili ujue wakati wanaponyunyizia<br>Waombe wakulima wanyunyizie dawa usiku wakati ambapo nyuki wamo mizingani |
| Mioto | Uchomaji wa vichaka | Kata nyasi na vichaka vilivyo karibu na sehemu uliyofuga nyuki wako |

**Kwa habari zaidi, wasiliana na:**

## Njia ya kufikia soko:

National Apiculture Development Organisation (TUNADO)
S.L.P: 5318 Kampala-Uganda
Simu: +256-41-343160, Barua pepe: tunadobee@yahoo.co.uk

Honey Care Kenya Limited
S.L.P: 24487-00502, Nairobi, Kenya.
Simu/Nukunishi: +254-20-3874448/50
Barua pepe: info@honeycareafrica.com, Gombowavu: www.honeycareafrica.com

Africa Now Kenya Limited
S.L.P : 2514, Kisumu Kenya
Simu/nukunishi: +254-57-2021181
Barua pepe: kisumu@africanow.org, Gombowavu: www.africanow.org

## Njia ya kufikia wafunzao:

Bee Natural Products Uganda Ltd
S.L.P.: 5318, Pan Africa House, Ploti 3 Kimathi Avenue
Kampala, Uganda
Simu: +256-41-253844 or 234676; Nukunishi: +256-41-259052
Gombowavu: www.beenaturalproducts.com

International Centre for Insect Physiology and Ecology (ICIPE)
S.L.P.: 30772-00100, Nairobi, Kenya
Simu: +254 (20) 8632000; Nukunishi: +254 (20) 8632001/8632002
Barua pepe: icipe@icipe.org; Gombowavu: www.icipe.org

National Agricultural Advisory Services (NAADS)
S.L.P. 25235, Kampala, Uganda
Simu: +256-41-345440/345065/345066; Nukunishi: +256-41-347843
Barua pepe: naads@iwayafrica.com; Gombo wavu: www.naads.or.ug

Sasakawa Global 2000 (MoA)
S.L.P.: 62347, Addis Ababa Ethiopia
Simu: +251-115-518040; Nukunishi: +251-115-512984 Barua pepe: moa@telecom.net.et

---

CTA

partageons les connaissances au profit des communautés rurales
sharing knowledge, improving rural livelihoods

ACP-EU Technical Centre for Agricultural and Rural Cooperation (CTA)
S.L.P 380, 6700 AJ Wageningen, The Netherlands
Simu: +31(0)317-467100, Kipepesi: +31(0)317-460067
Barua pepe: cta@cta.int, Wavuti: www.cta.int

CTA imedhaminiwa na jumuiya ya Ulaya

© CTA 2010 - ISSN 1877-6779

*Maelezo/ujumbe katika muongozo huu waweza kutolewa au kuchapishwa kwa matumizi yasiyo ya kibiashara iwapo utatambulisha kimetengezwa na CTA.*
*Kuchapishwa kwa manufaa ya biashara kunahitaji idhini kutoka kwa CTA.*